

### **Maelezo yanayohitaji tafsiri:**

Aina mpya ya Delta imethibitisha kuwa wakati wowote, visa vya COVID-19 vinaweza kuongezeka kighafla. Kupatia wafanyakazi wako ulinzi wa njia ya kupumua (N95) dhidi ya hatari za njia ya kupumua, kama vile virusi vinavyosababisha COVID-19, ni kiwango cha usalama kinachodhibitiwa na kutekelezwa na Washington Department of Labor and Industries (Idara ya Leba na Viwanda katika Washington). Kipimo cha usahihi huhakikisha kuwa kipumuzi cha N95 kitachuja 95% ya virusi vinavyosababishwa na hewa kikitumika vizuri. Waajiriwa wako waendeleo kufanya kazi kwa kuwapa kipumuzi kilichopimwa na kinatosha na tayari kutumika vizuri.

DOSH Directive 11.80 Temporary Enforcement Guidance (Mwelekeo wa 11.80 Mwongozo wa Utekelezaji wa Muda) (<https://lni.wa.gov/dA/1d2a778d31/DD1180.pdf>) (Kiingereza pekee) ulisasiswa Septemba 21, 2021. L&I itaanza kutekeleza mahitaji ya kipimo cha kila mwaka cha usahihi mnamo Januari 1, 2022. Hii inamaanisha, kwa mfano, ikiwa waajiriwa wako walipimwa usahihi mnamo 11/1/2020, watahitaji kupimwa tena usahihi kabla ya 11/1/2021. Wasipopimwa, kituo chako kinaweza kutajwa mnamo Januari 1, 2022 kwa kuttoa kipimo cha usahihi kila mwaka.

Sasa ndio wakati wa kutumia huduma ambazo Department of Health (DOH, Idara ya Afya) inatolea watoaji huduma ya utunzaji wanaowatunza wakazi/wateja waliojitenga au waliopo katika karantini - Tathmini ya kimatibabu na kipimo cha usahihi BILA MALIPO kwa matumizi ya kipumuzi. Ofa hii itaisha muda mwishoni mwa 2021.

Tembelea tovuti ya DOH Respiratory Protection Program (Mpango wa Ulinzi wa Njia ya Kupumua) website (<https://www.doh.wa.gov/ForPublicHealthandHealthcareProviders/HealthcareProfessionsandFacilities/HealthcareAssociatedInfections/RespiratoryProtectionProgram>) (Kiingereza pekee) ili kupata maelezo zaidi katika Respiratory Protection Program :: Washington State Department of Health, au tuma barua pepe kwa [HAI-FitTest@doh.wa.gov](mailto:HAI-FitTest@doh.wa.gov).